



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**KIKAO CHA THELATHINI**

**15 JULAI, 2010**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA THELATHINI – TAREHE 15 JULAI, 2010

### I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

#### WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI.

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 1 ya Mwaka 2009/2010 [*Statement of Reallocation Warrant No. 1 of the Year 2009/2010*].

### II. MASWALI:

#### OFISI YA WAZIRI MKUU:

231. MESHIMIWA GEORGE MALIMA  
LUBELEJE (MPWAPWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-  
Vijiji vya Lupeta, Bumila na Kimagai  
vilivyopo Kata ya Kimagai Wilayani  
Mpwapwa havina zahanati na hivyo  
kufanya wananchi wa vijiji hivyo kufuata  
huduma ya afya kwenye hospitali ya  
Wilaya ya Mpwapwa iliyopo umbali wa k.m  
kumi (10) hadi kumi na tano (15):-

Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani za  
ujenzi wa zahanati kwa ajili ya vijiji hivyo  
katika Bajeti ya Mwaka 2009/2010.

## **WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**

### **232. MHESHIMIWA JANET BINA KAHAMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa  
Mambo ya Nje na Ushirikiano wa  
Kimataifa:- Septemba mwaka 2009,  
Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipiga  
kura juu ya kuundwa kwa Shirika jipya  
lenye nguvu zaidi kwa ajili ya Wanawake  
na ambalo liliunganisha ofisi tatu za  
Umoja wa Mataifa zinazoshughulikia

masuala ya Wanawake kuwa chombo kimoja chini ya Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa; kwa kuwa hatua hiyo ya UN ni njia muafaka ya kutolea usawa na haki kwa Wanawake wote Duniani:-

Je, ni hatua gani zimefikiwa katika utekelezaji wa Azimio hilo la UN.

## **WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

### **233. MHESHIMIWA. MGENI JADI KADIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Serikali imeweka kipaumbele kwenye kilimo kupitia kaulimbiu ya Kilimo Kwanza:-

Je, kauli hiyo ina tofauti gani na Siasa ni Kilimo, Kilimo cha Kufa na Kupona na Kilimo ni Uti wa Mgongo.

## **WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

### **234. MHESHIMIWA ERNEST GAKEYA MABINA (GEITA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Serikali iliahidi kujenga nyumba pindi uongozi wa Wilaya ya Geita utakapopata viwanja kwa ajili ya waathirika wa Mgodhi Mpya ambao wanaishi kwenye mahema baada ya kushindwa kesi yao na Geita Gold Mine (GGM):-

Je, ni lini nyumba hizo zitajengwa.

### **235. MHESHIMIWA DK. RAPHAEL MASUNGA CHEGENI (BUSEGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Umeme wa Lamadi,

Kalemera, Nyamikoma, Nyakaboja hadi Nyashimo na ule wa Lamadi, Mkula Hospitali, Igalukilo, Malili hadi Ngasamo Ginnery na Nyashimo, Nyamatembe, Shighala, na Mwanangi, Badugu umekuwa uko ndani ya mpango wa Serikali kwa muda mrefu:-

- (a) Je, mradi huo utanza lini na kampuni gani imeteuliwa kutekeleza mradi huo;
- (b) Je, ni fedha kiasi gani imetengwa kwa ajili hiyo.

### **III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Kampuni Binafsi wa Mwaka 2010 [*The Public Private Partnership Bill, 2010*].

**DODOMA  
15 JULAI, 2010**

**DKT. T.D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**